P1 KISWAHILI

Insha mwongozo

1. Umetangazwa kuwa mwanafunzi bora katika mtihani wa kitaifa. Mwalimu mkuu wa shule ya upili ya Tangamano amekualika katika shule hii yake kuwahutubia wanafunzi kuhusu kilichochangia ufanisi wako. Andika **hotuba** utakayowatolea walimu,wazazi na wanafunzi wa shule hiyo.

   Kichwa lazima kiandikwe kwa herufi kubwa, kitaje neno hotuba, kipigiwe mstari mmoja akisitoneshwe hapo mwisho. - 4 mks
   Muundo uwe na mambo matano:
   Alama ya kunukuu isitumiwe-2mks
   Nafsi ya kwanza itumiwe-akitumia ya tatu asipite 04/20
   Awatambue waliohudhuria kulingana na vyeo kuanzia cheo cha juu. Akikosa asipite 08/20
   Maudhui yawe manane. Yakipungua manane asizidi 10/20
   Aya ya mwisho awashukuru waliohudhuria. Akikosa asizidi 12/20
   Baadhi ya hoja
   1. Nilisoma kwa bidii
   2. Nilifanya mitihani ya mara kwa mara
   3. Nilidurusu katika makundi
   4. Niliwahusisha walimu mara kwa mara
   5. Nilikamilisha silabasi kwa wakati
   6. Nilikuwa na utulivu shuleni
   7. Nilizingatia nidhamu
   8. Nilikuwa na vitabu vya kutosha
   9. Nilipata msaada mzuri wa wazazi (kadiria hoja za mtahiniwa)

Mtahiniwa akiwa hana **lugha** na hana **maudhui** kiwango chake ni 01-05
Mtahiniwa akiwa hana **lugha** japo ana **maudhui** kiwango chake ni 06-10
Mtahiniwa akiwa ana **lugha** na ana **maudhui** kiwango chake ni 11-15
Mtahiniwa akiwa ana **lugha, maudhui pamoja na umbuji na ustadi wa hali ya juu wa mapambo ya lugha na ubunifu,** kiwango chake ni 16-20

2. Wewe ni mwandishi wa habari. Umepata nafasi ya kumhoji waziri wa utalii kuhusu faida na hasara za utalii nchini. Andika **mahojiano** hayo.
   Kichwa lazima kiandikwe kwa herufi kubwa, kitaje neno mahojiano, kipigiwe mstari mmoja akisitoneshwe hapo mwisho. - 4 mks

Mtindo wa kitamthilia utumiwe. Mhusika mmoja aulize maswali na wa pili atupe majibu ya maswali hayo kiaya. Wote wakichangia huo ni upungufu wa kimtindo. Usimwadhibu mradi kuna alama.

**Baadhi ya maudhui**

**Faida**
Fedha za kigeni-aseme umuhimu wa fedha hizo. Asiposema asipite 10/20
Ajira na umuhimu wake
Barabara kuimarishwa
Hoteli kuboreshwa
Usalama kuimarika
Uhusiano mwema baina ya mataifa
**Hasara**
Tamaduni potuvu
Vijana kuacha shule
Ulanguzi wa dawa. Kila hasara iishie kwa suluhu.

**a. Maudhui**

a. Mtahiniwa aandike maudhui manane na zaidi
b. Aanze na maudhui mazito mazito
c. Maudhui yaandikwe kiaya
d. Aya iwe ya mraba / wima
e. Aya zisipungue kumi
f. Mstari mmoja urukwe kabla ya kuanza aya nyingine
g. Kila aya iwe na maudhui moja.
h. Maudhui yajadiliwe kwa kina
i. Maadili na urasmi wa lugha vizingatiwe na kudumishwa.
j. Maudhui yajitokeze wazi hasa katika sentensi ya kwanzakwenye kila aya
k. Vidokezo viorodheshwe katika sehemu yenye maswali.
l. Aya iwe kati ya mistari 5-7, au maneno 40-50
m. Katika swali linalohitaji suluhisho, suluhisho hilo lijitokezekatika kila sentensi ya mwisho kwenye kila aya. Iwapomaudhui ni manane basi suluhu pia ni nane.
n. Uhalisia uzingatiwe hasa katika insha 1 na 2
o. Katika swali lililo na sehemu mbili, faida na hasara, zote ziangaziwe na msimamo kutolewa katika aya ya mwisho, (6,2 au 5,3) kwa kuegemea hoja nyingi, si 4,4 au 7,1,au 8,0

**c. Mtindo**

- Mtahiniwa afahamu sura ya insha zote za kiuamilifu. Lazimaafahamu umbo la kila aina ya insha.
- Azingatie urefu zaidi ya kurasa 4 au maneno 400

- Azingatie **nyakati** kulingana na aina ya insha.
- Azingatie **nafsi / ajihusishe** kulingana na aina ya insha.
- **Unadhifu** wa insha uzingatiwe. Kazi safi humpendezamtahini. Kazi chafu humkwaza na kumtamausha mtahini.
- Asikatekate silabi kiholela, kwa mfano, katik-a, badala yakati-ka. Konsonanti na irabu zisitenganishwe.
- Aonyeshe **nambari** ya insha anayojibu kikamilifu.
- Aandike **herufi vizuri** bila kuzishikanisha na kwa utaratibu.
- Atoneshe herufi **i** na **j** vizuri
- Asitenganishe maneno visivyo, k.m aliye kuja badala ya aliyekuja, nime kuadhibu badala ya nimekuadhibu.
- Akumbuke kuwa palipo na 'o' rejeshi kwenye kitenzi, nenohilo na moja si mawili. Kwa hivyo asitenganishe. Kwamfano, lilil**o**potea wala si lili**lo** potea
- **Asiunganishe** maneno visivyo, kwa mfano kwa sababu badala ya kwa sababu
- Mtahiniwa asidondosha herufi Katika neno, kwa mfano aandike **kibia** badala ya **kimbia**,
- Mtahiniwa aepuke kupachika ama kuongeza herufi katika neno. Kwa mfano aandike **muku**tano badala ya kuandika **mku**tano.
- Kubadilisha herufi za neno pia ni kosa. Kwa mfano aandikeneno sigilisa badala ya sikiliza,
- Matumizi ya **tarakimu** yawe nadra. Atumie mneno badala ya tarakimu kwa wingi.
- Vifupisho viepukwe-k.m,k.v.m.f,n.k,
- Mtiririko na mshikamano wa **mawazo kiaya** na katika inshanzima uonekane.
- Hati **nzuri** na inayosomeka kwa urahisi itumiwe.
- Wino wa **samawati** utumiwe.
- Sentensi **komavu** na zenye mnato zitumiwe kwa wingi.
- Insha zote sharti ziwe na kichwa

**b. Maudhui**

p. Mtahiniwa aandike maudhui manane na zaidi
q. Aanze na maudhui mazito mazito
r. Maudhui yaandikwe kiaya
s. Aya iwe ya mraba / wima
t. Aya zisipungue kumi
u. Mstari mmoja urukwe kabla ya kuanza aya nyingine
v. Kila aya iwe na maudhui moja.
w. Maudhui yajadiliwe kwa kina
x. Maadili na urasmi wa lugha vizingatiwe na kudumishwa.
y. Maudhui yajitokeze wazi hasa katika sentensi ya kwanzakwenye kila aya
z. Vidokezo viorodheshwe katika sehemu yenye maswali.
aa. Aya iwe kati ya mistari 5-7, japo katika utangulizi na tamatiiwe mistari 2-4
bb. Katika swali linalohitaji suluhisho, suluhisho hilo lijitokezekatika kila sentensi ya mwisho kwenye kila aya. Iwapomaudhui ni manane basi suluhu pia ni nane.
cc. Uhalisia uzingatiwe hasa katika insha 1 na 2
dd. Katika swali lililo na sehemu mbili, faida na hasara, zote ziangaziwe na msimamo kutolewa katika aya ya mwisho, (6,2 au 5,3) kwa kuegemea hoja nyingi, si 4,4 au 7,1,au 8,0

**c. Mtindo**

- Mtahiniwa afahamu sura ya insha zote za kiuamilifu. Lazimaafahamu umbo la kila aina ya insha.
- Azingatie urefu zaidi ya kurasa 2 ½ au maneno 400

- Azingatie **nyakati** kulingana na aina ya insha.
- Azingatie **nafsi / ajihusishe** kulingana na aina ya insha.
- **Unadhifu** wa insha uzingatiwe. Kazi safi humpendezamtahini. Kazi chafu humkwaza na kumtamausha mtahini.
- Asikatekate silabi kiholela, kwa mfano, katik-a, badala yakati-ka. Konsonanti na irabu zisitenganishwe.
- Aonyeshe **nambari** ya insha anayojibu kikamilifu.
- Aandike **herufi vizuri** bila kuzishikanisha na kwa utaratibu.
- Atoneshe herufi **i** na **j** vizuri
- Asitenganishe maneno visivyo, k.m aliye kuja badala ya aliyekuja, nime kuadhibu badala ya nimekuadhibu.
- Akumbuke kuwa palipo na 'o' rejeshi kwenye kitenzi, nenohilo na moja si mawili. Kwa hivyo asitenganishe. Kwamfano, lili**lo**potea wala si lili**lo** potea
- **Asiunganishe** maneno visivyo, kwa mfano kwa sababu badala ya kwa sababu
- Mtahiniwa asidondosha herufi Katika neno, kwa mfano aandike **kibia** badala ya **kimbia**,
- Mtahiniwa aepuke kupachika ama kuongeza herufi katika neno. Kwa mfano aandike **muku**tano badala ya kuandika **mku**tano.
- Kubadilisha herufi za neno pia ni kosa. Kwa mfano aandikeneno sigilisa badala ya sikiliza,
- Matumizi ya **tarakimu** yawe nadra. Atumie mneno badala ya tarakimu kwa wingi.
- Vifupisho viepukwe-k.m,k.v.m.f,n.k,
- Mtiririko na mshikamano wa **mawazo kiaya** na katika inshanzima uonekane.
- Hati **nzuri** na inayosomeka kwa urahisi itumiwe.
- Wino wa **samawati** utumiwe.
- Sentensi **komavu** na zenye mnato zitumiwe kwa wingi.